

DONDOO ZA UJENZI WA BANDA BORA LA NG'OMBE

June 23, 2019 IBRAHIM




DONDOO

ZA UJENZI WA BANDA BORA LA NG'OMBE

DONDOO ZA UJENZI WA BANDA BORA LA NG'OMBE : Idadi kubwa ya wafugaji hawatilii maanani umuhimu wa nafasi, ukubwa na idadi ya wanyama wanaopaswa kuwa ndani wakati wa ujenzi wa mabanda. Hujenga mabanda madogo kiasi cha kuwanyima uhuru wanyama kuzunguka ndani au kukidhi mahitaji yao ya kitabia pale wanyama husika wawapo ndani ya mabanda hayo.

Ujenzi wa banda siyo tu kuunganisha kwa kupigilia misumari magome ya miti au mbaao kama wengi wanavyochukulia, ni shughuli inayogharimu na mfugaji anapasa kuepuka makosa wakati wa ujenzi kwa kufi kiria mambo mbalimbali muhimu kulingana na mahitaji ya ng'ombe wake.

- Banda la ng'ombe ni vema likajengwa karibu na chanzo cha uhakika cha maji na kama ikiwezekana liwe karibu na shamba la malisho.
- Paa lake linaweza kuenezwa eneo zima la banda au sehemu wanayolala wanyama tu pia liwe na mteremko kuanzia kwenye banda lenyewe kuelekea sehemu ya nje ili kuzuia maji ya mvua yasiweze kuingia bandani. Vilevile liwe na urefu wa kiasi cha mtu mzima kuweza kusimama ndani.
- Sakafu ya sehemu inayoruhusu wanyama kutembea iwe imetengenezwa kwa zege au udongo ulioshindiliwa vyema. Sakafu ya zege itarahisisha usafi shaji na sakafu iwe na imeinama kiasi kuelekea kwenye mfereji unaoelekea kwenye shimo la samadi,
- Sakafu ya sehemu ambayo wanyama hupitia iwe imetengenezwa kwa zege au udongo ulioshindiliwa vyema. Sakafu ya zege itarahisisha usafi shaji na iwe na mwinamo kiasi kuelekea kwenye mfereji unaoelekea kwenye shimo la samadi, nje ya banda na isiwe inateleza ili kuepusha ng'ombe wako wasiteleze.



MCHORO UNAONYESHA NAMNA BANDA BORA LINAVYOPASWA KUJENGWA

- Kuweza kuhifadhi vyema samadi, mfugaji anapasa kuchimba shimo kubwa la samadi na pia kusakafia mfereji unaopeleka samadi hiyo kutoka sehemu wanayopumzikia ng'ombe hadi kwenye shimo hilo.
- Unaweza kutengeneza tope kwa mchanganyiko wa udongo mwekundu, samadi na majivu na kusakafia shimo hili upande wa chini na pembezoni na uache ikauke na rudia mchakato huu mara tano ili kulifanya shimo lako lisivujishe samadi.
- Kila ng'ombe anapasa kuwa na Kijichumba chake (cubicle) ndani ya banda. Sakafu ya vijichumba hivyo zifanywe kwa udongo mkavu kwa sababu ng'ombe hupenda kulala sehemu ya udongo kuliko sakafu ya zege ambayo kwa kawaida huwa ni ya baridi.
- Kwa upande wa ndama banda lao linaweza kutengenezwa kuzungushiwa uzio wa muda kwa kutumia magome ya miti au mbao na kutengeneza vijichumba vidigovidogo kwa ajili ya kulala. Sakafu ya vijichumba hivi vijengewe vichanja vya miti vilivyoinuliwa kiasi cha sentimita 4 kutoka ardhini ili kuhakikisha kunakuwa na hali ya usafi wakati wote na hivyo kuwaepusha ndama wako kuwa salama dhidi magonjwa mbalimbali.
- Banda litakalotumika kama sehemu ya kukamuliwa ni vyema likawa mbali na mahali lilipo banda hili.

- Weka manywesheo na malishio sehemu wanayopita ng'ombe na kwenye banda la ndama na pia malishio mengine yawekwe kwenye banda la kukamulia ili ng'ombe wako waendelea kula wakati wakikamuliwa maziwa

MCHORO WA BANDA DOGO KWA AJILI YA NG'OMBE WACHACHE

